

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA SITINI NA MOJA

29 JUNI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA SITINI NA MOJA – TAREHE 29 JUNI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

510. **MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara ya kutoka Ilembo hadi Itenka ni Barabara muhimu Kiuchumi:-

Je, ni lini Serikali itaifanyia ukarabati Barabara hii.

511. **MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Mradi wa Ujenzi wa Soko la Kisasa katika Halmashauri ya Mji wa Tarime wenye thamani ya Shilingi Bilioni 8.07 utakamilika.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

512. MHESHIMIWA DKT. STEPHEN LEMOMO KIRUSWA (LONGIDO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa kipande cha Barabara ya lami kilichoanzia Sanya Juu kuelekea Kamwanga mpaka Kijiji cha Elerai takribani Kilomita 44 ili kuunganisha na kipande cha lami kinachotoka Tarakea na kuishia Kijiji cha Kamwanga.

513. MHESHIMIWA SIMON SONGE LUSENGEKILE (BUSEGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya kutoka Nyashimo Wilayani Busega hadi Dutwa Wilayani Bariadi kupitia Shigala, Malili, Ngasamo na Imalamate yenye Kilomita 47 kwa kiwango cha lami.

514. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kolandoto – Oldean Junction utaanza kwa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulishafanyika.

WIZARA YA MAJI:

515. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

- (a) Je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Kata za Kigwa, Goweko, Igalula na Nsololo;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa uchimbaji wa Mabwawa katika Kata za Mmale, Miswaki, Lutende na Kizenga ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji katika maeneo hayo.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**516. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN
ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina Mikakati gani ya kuanza uzalishaji katika Kiwanda cha Chuma Mang'ula.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**517. MHESHIMIWA HASSAN SELEMANI
MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Serikali itanza ukarabati wa Hospitali ya Mkoa wa Mtwara.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

518. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Kumekuwa na kawaida kwa baadhi ya Taasisi za Serikali kutotumia huduma za Shirika la Bima la Zanzibar kwa kisingizio kuwa Shirika hilo siyo la Umma:-

- (a) Je, Serikali inalitambua Shirika hilo kama la Serikali au Shirika Binafsi;
- (b) Kama ni Shirika la Serikali, nini wito wa Serikali kwa Watendaji ambao wamekuwa wakikataa kutumia huduma hiyo kwa kisingizio cha kuwa siyo Shirika la Serikali.

DODOMA
29 JUNI, 2021

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE